



## East African Journal of Swahili Studies

eajss.eanso.org

Volume 5, Issue 1, 2022

Print ISSN: 2707-3467 | Online ISSN: 2707-3475

Title DOI: <https://doi.org/10.37284/2707-3475>



EAST AFRICAN  
NATURE &  
SCIENCE  
ORGANIZATION

Original Article

## Maongezi Katika Riwaya Za Kiswahili

*Daniel Kiprugut Ng'etich<sup>1\*</sup>, Richard Makhanu Wafula<sup>1</sup> na Joseph Nyehita Maitaria<sup>1</sup>*

<sup>1</sup> Chuo Kikuu cha Kenyatta; S. L. P. 43844-00100 Nairobi, Kenya.

\* ORCID ID: <https://orcid.org/0000-0002-0963-7150>; Barua pepe ya mawasiliano: [ngetichdkiprugut@gmail.com](mailto:ngetichdkiprugut@gmail.com)

DOI ya Nakala: <https://doi.org/10.37284/jammk.5.1.781>

Tarehe ya Uchapishaji: **IKISIRI**

08 Agosti 2022

**Istilahi Muhimu:**

*Maongezi,  
Riwaya ya Kiswahili,  
Uainishaji,  
Dhima,  
Ukuaji.*

Makala hii inaangazia dhima ya maongezi katika riwaya ya Kiswahili. Riwaya ni mojawapo wa tanzu muhimu za fasihi ya Kiswahili ambayo inaendelea kukua kwa upande wa wahusika, dhamira, maudhui, mtindo na upeo. Utanzu wa riwaya ya Kiswahili ulianza mwanzo wa karne ya ishirini wakati James Juma Mbotela alipoandika riwaya ya Uhuru wa Watumwa (1934). Ukuaji wake umeshika kasi zaidi katika mwongo wa mwisho wa karne ya ishirini na mwanzo wa karne ya ishirini na moja. Ni muhimu pia kutambua kuwa, utungaji wa riwaya umeendelea kukua sambamba na uhakiki wake. Katika karne ya ishirini na moja, riwaya ya Kiswahili imefikia utungaji wa kimajaribio (Mwamzandi, 2013:48-66 na Mohamed 2003:78-79). Katika riwaya za kimajaribio, watunzi hujumuisha nadharia, visasili pamoja na kuzungumzia masuala ya utandawazi na soko huru. Ni riwaya ambazo hukiuka miundo ya riwaya iliyozoeleka. Kwa upande wa maongezi, usemaji wa wahusika katika riwaya umekua kutoka sahili hadi changamano kutokana na masuala yanayojadiliwa katika riwaya mahususi. Ni maoni ya waandishi wa makala hii kuwa, usemaji wa wahusika unaweza kuathirika na vipindi vya kihistoria hivyo basi kuwa na mchango muhimu katika maendeleo ya riwaya. Madhumuni ya makala hii ilikuwa ni kuainisha maongezi katika riwaya za Kiswahili. Riwaya ambazo zilichanganuliwa kwa mujibu wa makala hii ni Kusadikika (1951), Mafuta (1984) na Kufa Kuzikana (2003). Riwaya hizo ziliteuliwa kuwakilisha vipindi mahususi vya ukuaji na maendeleo ya riwaya ya Kiswahili. Makala hii iliongozwa na nadharia ya Uchanganuzi wa Usemi Hakiki. Kutokana na uchanganuzi huo, makala hii imebainisha mchango wa maongezi kwa ukuaji, maendeleo na uumbufu wa utanzu wa riwaya kwa ujumla.

#### APA CITATION

Ng'etich, D. K., Wafula, R. M. & Maitaria, J. N. (2022). Maongezi Katika Riwaya Za Kiswahili. *East African Journal of Swahili Studies*, 5(1), 224-233. <https://doi.org/10.37284/jammk.5.1.781>.

#### CHICAGO CITATION

Ng'etich, Daniel Kiprugut, Richard Makhanu Wafula and Joseph Nyehita Maitaria. 2022. "Maongezi Katika Riwaya Za Kiswahili". *East African Journal of Swahili Studies* 5 (1), 224-233. <https://doi.org/10.37284/jammk.5.1.781>.

#### HARVARD CITATION

Ng'etich, D. K., Wafula, R. M. & Maitaria, J. N. (2022) "Maongezi Katika Riwaya Za Kiswahili", *East African Journal of Swahili Studies*, 5(1), pp. 224-233. doi: 10.37284/jammk.5.1.781.

#### IEEE CITATION

D. K. Ng'etich, R. M. Wafula & J. N. Maitaria, "Maongezi Katika Riwaya Za Kiswahili", *EAJSS*, vol. 5, no. 1, pp. 224-233, Aug. 2022.

#### MLA CITATION

Ng'etich, Daniel Kiprugut, Richard Makhanu Wafula & Joseph Nyehita Maitaria "Maongezi Katika Riwaya Za Kiswahili". *East African Journal of Swahili Studies*, Vol. 5, no. 1, Aug. 2022, pp. 224-233, doi:10.37284/jammk.5.1.781.

## UTANGULIZI

Tangu chimbuko lake, riwaya ya Kiswahili imekuwa na kubadilika kimtindo na kimaudhui. Riwaya za mwanzo mwanzo kama zile za Shaaban Robert ziliangazia sana maudhui ya maadili katika jamii. Riwaya hizo ni kama vile: *Kusadikika* (1951), *Adili na Nduguze* (1951), *Kufikirika* (1967), *Siku ya Watenzi Wote* (1968) na *Utubora Mkulima* (1968). Baada ya uhuru, riwaya iliendelea kukua zaidi na kushughulikia maudhui changamano kwa mujibu wa jamii ya wakati huo. Kufikia miaka ya 1970, riwaya nyingi zilianza kujishughulisha na masuala kama vile: uongozi mbaya, ukoloni mamboleo, usaliti wa kisiasa, unafiki na utawala wa kiimla. Riwaya zilianza kuwa za kihalisia zaidi na zikashughulikia mambo yaliyoibuka katika nchi huru za Afrika Mashariki. Katika kipindi cha karne ya ishirini na moja, riwaya ya Kiswahili inashughulikia masuala ya soko huru na utandawazi kama ilivyo katika riwaya ya *Babu Alipofufuka* (Mohamed, 2001). Aidha, kuna riwaya ambazo zimejikita katika masuala ya kinadharia kama vile: *Dunia Yao* (Mohamed, 2006) na *Nagona* (Kezilahabi, 1990). Kwa mujibu wa Mohamed (2007), mbali na riwaya ya Kiswahili kuathiriwa kimabadiliko ndani na nje ya miundo ya utanzu wenyewe, utanzu wa riwaya kwa kawaida ni regerege na tepetepe, wenye kugeukageuka na kubadilika. Maoni haya yanadhihirisha kuwa, riwaya ya Kiswahili ni nyumbufu na badilifu. Bado ipo katika umbo ambalo litaendelea kubadilika kwa mujibu wa mageuko ya kiwakati. Ni maoni yetu kuwa, kwa kuwa maongezi ni mojawapo wa

vipengele vinavyojenga riwaya, yamekuwa yakikua na kubadilika kadri riwaya ya Kiswahili inavyoendelea kukua. Madai yetu ni kwamba, kwa kuwa wahusika wa riwaya za mwanzo mwanzo katika fasihi ya Kiswahili walikuwa na dhima ya kuendeleza maudhui ya maadili; mwandishi alieleza maadili hayo kwa kuwatumia kutongoa kauli teule badala ya kuwapa nafasi ya kuyaigiza maadili yao kupitia katika maongezi. Makala hii inauia kuonyesha kwamba, riwaya ya Kiswahili imepevuka kutokana na matumizi ya mazungumzo anuwai na changamano.

Maongezi ya kifasihi ni mazungumzo ambapo msomaji anaweza kuwachunguza watu wanaozungumza na yale wanayoyasema, tofauti zao na masuala yanayoibuka katika mazungumzo yao. Maongezi yanaibua mahusiano ya sehemu nne: kati ya mhusika na mhusika, mhusika na msimulizi, maendeleo ya mazungumzo na matini yenyewe na kati ya matini ya fasihi na msomaji. Kwake, maongezi kutokana na hali yake ya usemi halisi humpa msomaji nafasi ya kujihusisha moja kwa moja na yaliyomo bila kutegemea maelezo ya msimulizi. Matumizi ya maongezi humfanya mwandishi kuwa zaidi ya msimulizi kwani huwaruhusu wahusika kuzungumza. Maongezi pia huendeleza mgogoro na msuko wa matukio katika kazi ya fasihi husika (Haines, 1991). Maoni haya ya Haines yanabainisha kuwa, maongezi ni sehemu muhimu katika kukuza na kuendeleza kazi ya fasihi. Ni maoni yetu kuwa, maongezi katika riwaya ya Kiswahili yamekuwa yakibadilika ili kuendeleza mgogoro na msuko katika riwaya ya Kiswahili.

Kulingana na Hawthorn (1992), sauti mbalimbali huwakilisha na kuwasilisha mitazamo mahususi. Akimrejelea Bakhtin anadai kuwa, sauti tofauti tofauti katika riwaya zinaweza kutenganishwa. Tunapozungumza, matamshi yetu huwa na sauti tofauti tofauti na kila sauti hubeba itikadi zake. Hii ina maana kuwa, kila tamko linaweza kuwa na mitazamo maalum. Mtunzi wa riwaya hufuata njia zilizozeleka katika kuwasilisha usemi na maongezi ambayo kwayo tunaweza kuona kama maongezi ya kawaida tu baina ya binadamu. Mtunzi huwasilisha kwa maneno yale ambayo katika mazungumzo ya kawaida yangehusisha: kiimbo, kusitasita, ishara, mkaofu wa mwili na mitindo mingine.

Makala hii itaonyesha tofauti ya maongezi katika riwaya za 1950 hadi 1970 na zile za miaka ya 1980 hadi sasa. Tutatoa mifano kutoka, *Kusadikika* (Shaaban, 1951), *Utubora Mkulima* (1968), *Mafuta* (Mkangi, 1984) na *Kufa Kuzikana* (Walibora, 2003). Baadaye, tutafafanua dhima ya maongezi katika riwaya ya Kiswahili ya 1990 hadi sasa.

### MISINGI YA NADHARIA

Data ilichanganuliwa kwa kuzingatia mihimili ya nadharia ya Uchanganuzi wa Usemi Hakiki. Nadharia ya Uchanganuzi Usemi Hakiki inahusishwa na wataalamu wafuatao: Theo van Leeuwen, Gunther Kress, Teun van Dijk, Ruth Wodak na Norman Fairclough (Wodak, 2001). Ni nadharia ambayo inachanganua mahusiano yaliyopo kati ya jinsi lugha inavyotumiwa na miktadha ya kijamii na kisiasa ambapo lugha husika inatumika (Paltridge, 2006:179). Ni nadharia ambayo hushughulikia jinsi masuala kama vile jinsia, utamaduni, itikadi na ukabila huakisiwa katika matini. Aidha, nadharia ya Uchanganuzi wa Usemi Hakiki huchunguza jinsi mahusiano ya kijamii hujenga lugha au kujengwa na lugha. Waandishi wa fasihi huwasawiri wahusika wanaotekeleza shughuli zao katika miktadha mahususi. Usemaji wa wahusika unaathirika na matukio ya kijamii, kisiasa na kitamaduni kulingana na yaliyomo katika mazingira hayo.

Kulingana na Fairclough (1992:90), itikadi za jamii au mwandishi hupatikana katika matini. Hivyo, si rahisi kutenganisha matini na itikadi. Maana katika matini hutokana na fasiri anuwai ambazo huweza kutofautiana kiitikadi. Watumiaji wa lugha hutumia

lugha yao kwa mujibu wa miundo ya kitamaduni, kijamii na kihistoria. Wahusika katika riwaya ni viwakilishi vya watu hasi katika jamii. Kupitia usemaji wa wahusika hao mtunzi anaweza kubainisha itikadi za jamii husika. Akiendeleza suala la itikadi, van Dijk (1998:8), anaeleza kuwa, itikadi huathiri kinachochukuliwa kuwa ukweli au uwongo hasa ikiwa ni imani zinazoonekana kuwa muhimu kwa kikundi mahususi. Hivyo, itikadi hutawala mwono ulimwengu wa wanakikundi maalum. Usemaji wa wahusika katika riwaya hudhibitiwa na thamani za jamii zao hivi kwamba msimamo wao kuhusu masuala fulani huathiriwa na imani za jamii husika.

Nadharia ya Uchanganuzi wa Usemi Hakiki inadhihirisha jinsi baadhi ya wanajamii wanavyohalalisha matendo yao. Kwa mujibu wa van Leeuwen (2008:105-106), kuna njia kadhaa zinazotumika kuhalalisha matendo katika jamii. Anafafanua njia nne zinazotumiwa na wanajamii ili kuhalalisha wanayoyatenda. Njia ya kwanza ni ile ya kutumia mamlaka kwa kuamuru au kuruhusu. Njia hiyo inatekelezwa kwa kurejelea utamaduni, mila, sheria au watu wenye mamlaka katika jamii. Aidha, uhalalishaji unaweza kutekelezwa kwa kutathmini maadili. Katika njia hiyo, mambo yanayothaminiwa na wanajamii hurejelewa. Pia, malengo na umuhimu wa kutekeleza tendo fulani huweza kutumika kuhalalisha utendaji wa jambo mahususi. Kadhalika, matendo yanahalalishwa kupitia simulizi zinazoishia kwa kutuzwa kwa matendo yaliyohalalishwa na kuadhibiwa kwa yale yasiyohitajika.

Mihimili ifuatayo ya nadharia ya Uchanganuzi Usemi Hakiki ilitufaa katika uandishi wa makala hii:

- Usemi hutumiwa kwa lengo la kuendeleza masuala mahususi yanayothaminiwa na jamii husika. Kwa mfano, katika riwaya za miaka ya 1950, suala lililoendelezwa zaidi na watunzi wa kipindi hicho lilikuwa uadilifu.
- Mahusiano ya kimamlaka yanajadiliwa na kutekelezwa kupitia usemi. Hali hiyo inaweza kutathminiwa kwa kuchunguza ni nani ndiye anayadhibiti mazungumzo na anawaruhusu watu wepi kuzungumza. Wanajamii huhalalisha

matendo yao kwa kutumia mbinu mahususi ili kuonyesha kuwa, yale wanayoyatenda ni halali.

- Usemi unaakisi na kuibua mahusiano ya kijamii. Hii inamaanisha kuwa, mahusiano ya kijamii yanajengwa na kudumishwa kupitia maongezi.
- Itikadi inaasisiwa na kuonekana kupitia kwa matumizi ya usemi. Hii hujumuisha jinsi jamii inavyogawika kupitia mahusiano ya kimamlaka, kijinsia, kitabaka na kikabila.

Nadharia ya uchanganuzi wa usemi inalenga kubainisha yanayosemwa na kufanywa na watu kupitia usemi, kwa kulinganisha na mtazamo wao kuhusu; ulimwengu na kujihusu wenyewe. Kijumla nadharia hii ilisaidia kufafanua maongezi mahususi na kubainisha mbinu za kuibua, kukuza na kuendeleza maongezi katika riwaya teule.

## MAONGEZI YA RIWAYA KATIKA MPITO WA WAKATI

Riwaya za miaka ya 1950 hadi 1970 ziliupa usimulizi nafasi kubwa. Maongezi kati ya wahusika hayakutokea mara nyingi. Hata hivyo, maongezi yalipotumika aghalabu yalilenga kujenga wasifu wa mhusika. Kupitia maongezi hayo, mwandishi alibadilisha mazingira ya wahusika wake na kuibua hisia na usemaji ambao uliambatana na mazingira hayo. Pia, maongezi mengi yaliyotokea yalizungumzia suala moja kwa muda mrefu. Hali hii ni tofauti katika riwaya nyingi za kisasa ambapo mada za maongezi hubadilikabadilika ili kujenga maudhui mahususi na kukuza uchanganuzi wa msuko. Katika riwaya ya *Utubora Mkulima* (Shaaban, 1968), mtunzi anawasilisha aina ya maongezi ya kuzungumzia suala moja kwa kipindi kirefu katika sura ya riwaya. Kwa mfano, kutoka ukurasa wa kwanza hadi wa saba maongezi yote yanayotokea ni kati ya mhusika Utubora na Bwana Ahmed kuhusu nia ya Utubora kuacha kazi. Haya maongezi yanadhamiriwa kumjenga mhusika mkuu, Utubora. Lengo ni kumsawiri Utubora kama mhusika mwadilifu na wa kutegemewa kazini. Pia, mwandishi anaonyesha muumano kati ya Utubora na mwajiri wake. Hii ni kwa sababu suala la Utubora kutaka kuacha kazi linamtatiza sana Bwana Ahmed moyoni mwake. Kulingana na Rogers (2004:10), nadharia ya Uchanganuzi wa Usemi Hakiki inaanza kwa chukulizi kwamba matumizi ya

lgha hujengwa kwa miktadha ya kijamii, kitamaduni, kisiasa na kiuchumi. Hivyo uchanganuzi wa maongezi katika riwaya za kimaadili kama vile; *Kusadikia* (1951), *Adili na Nduguze* (1952) na *Utubora Mkulima* (1968) zina wahusika waliopewa usemaji unaobainisha maadili mahususi.

Maongezi ya kuzungumzia suala moja kwa kipindi kirefu, yalifanya riwaya husika kuwa na msuko sahili. Aghalabu mawazo machache mno yalikuzwa na mtiririko wa riwaya kuanzia mwanzo hadi mwisho wake ukawa wa moja kwa moja. Katika riwaya ya *Kusadikika* (1951), maongezi yanatokea kwa njia ya hotuba. Karama anapewa nafasi kubwa riwayani kujitetea dhidi ya mashtaka yaliyokuwa yakimkumba. Hata hivyo, ni wazi kuwa katika kujitetea kwake, anajaribu kudhihirisha hali ya uongozi mbaya wa utawala wa Kusadikika. Maongezi katika riwaya ya *Kusadikika* yanatokea kati ya wahusika watatu pekee: Karama, Majivuno na Mfalme. Ni bayana kuwa maongezi ya wahusika hawa yanarejelea suala moja kuu ambalo ni uongozi wa Kusadikika. Uchache wa maudhui yaliyozungumziwa na wahusika katika riwaya ulisababisha kuwepo kwa maongezi sahili. Usemaji Karama uliongozwa na muktadha wa kidhalimu katika jamii ya Kusadikika. Hivyo, hotuba yake inajadili dhana ya uanasheria na umuhimu wa kuanzisha elimu hiyo kwa Wanakusadikika. Katika riwaya ya *Kusadikika*, uongozi wa mfalme Jalali uliwafanya Wanakusadikika kuamini kuwa, nafasi yao katika uongozi ilikuwa duni. Kwa mujibu wa Bolinger (2014), lugha inaweza kuwa njia ya kudhibiti watu na kuathiri wanavyofikiria na kutenda. Wanakusadikika wanadhhibitiwa hivi kwamba, wanasadiki hali yao duni. Wanaona upinzani dhidi ya sheria dhalimu kama ukiukaji wa maadili. Hali hiyo inaonekana kupitia kauli ya Majivuno:

*Jalali Mfalme na madiwani wakuu wa baraza. Nataka kuweka mbele yenu mashtaka ya serikali ya Kusadikika juu ya Karama, raia mmoja, anayelindwa na ulinzi wa Mfalme, lakini si mwaminifu; anayefaidi haki na mapendeleo ya utawala huu, lakini si mtii ...* (Shaaban, 1951:1).

Usemaji wa Majivuno katika nukuu unaonyesha jinsi Wanakusadikika walivyofaa kufikiria. Hawakufaa kupinga sera za utawala kwa kuwa,

walipata ulinzi na haki kutoka kwa mfalme. Kauli kama hiyo inatumiwa kuhlalisha utawala wa kidhalimu kwa kudumisha hali iliyokuwepo. Unukuzi huo katika dondoo unathibitisha kuwa, riwaya za awali katika fasihi ya Kiswahili zilisisitiza zaidi suala la uadilifu. Hivyo, mhusika Majivuno anamwona Karama kama mtovu wa uadilifu kwa kutaka kuanzisha elimu ya uanasheria. Kutokana na waandishi kuwapa wahusika usemaji unaohusiana na uadilifu, mawanda ya yaliyorejelewa yalikuwa finyu na kuifanya riwaya kuwa sahili. Aidha, lugha anayotumia Majivuno inadhihirisha itikadi za watawala dhidi ya watawaliwa. Kulingana na Celce-Murcia na Olshtain (2000:10), nadharia ya Uchanganuzi wa Usemi Hakiki inadengua na kubainisha mahusiano yasiyo ya usawa katika jamii. Pia, huonyesha jinsi mahusiano hayo yanavyowasilishwa, yanavyoundwa na yanavyohalalishwa kupitia lugha. Usemaji wa Majivuno unaonyesha kuwa, Wanakusadikika walitegemewa kufuata masharti ya uongozi wa nchi yao bila kuonyesha dalili zozote za upinzani. Itikadi kama hizo ziliathiri mwonoulimwengu wa wahusika kwa kuwa, wangeamini kuwa, kupinga utawala ilikuwa ishara ya kukosa shukrani na uaminifu.

Isitoshe, maongezi katika riwaya za awali za Kiswahili yalitumiwa kujenga sifa za wahusika. Kwa mfano, Mhusika Karama anasawiriwa kuwa mwadilifu kupitia usemaji wake. Anapomjibu Majivuno, anadhihirisha heshima katika usemi wake, licha ya kuwa Majivuno alikuwa akimdhulumu kupitia mashtaka dhidi yake:

*Elimu ilipokuwa haijulikani duniani, mvi zilihesabiwa kuwa alama ya hekima. Fikira hii ilikuwa njema sana, lakini wakati wake umepita na haurudi tena. Sasa kama mtu hakuelimishwa, mvi zake hazihesabiwi kuwa dalili ya hekima. Jambo lisilobadilika ni kila mzee anastahili heshima ya kila kijana siku zote* (Shaaban, 1951:10).

Nukuu katika dondoo inaendelea sifa ya uadilifu anayopewa Karama. Usemaji huo hauonyeshi ukali dhidi ya anayemdhulumu. Licha ya Karama kupendelea elimu ya uanasheria, hakutaka kumvunja moyo Majivuno. Hivyo anamweleza kuwa, mvi ilikuwa ishara ya heshima – na ilikuwa njema. Katika harakati za watunzi kumkuza

mhusika mwadilifu, waliwakuza pia wahusika waovu waliokuwa mahasidi wao. Wahusika waovu walipewa usemaji uliodhihirisha hulka kama vile kiburi na ukatili. Kwa mfano, Majivuno anasawiriwa kama mwenye kubagua watu kwa sababu ya umri. Anasema yafuatayo kuhusu Karama:

*Mshtakiwa ana maneno mengi kama kitabu. Nakanusha kuwa ajua kitu chochote juu ya hekima. Hekima ni kitu adimu kupatikana na mtu asiye na mvi. Weusi wa nywele za mshtakiwa waonyesha waziwazi ujinga alio nao...* (Shaaban, 1951:10).

Nukuu katika dondoo ni mfano wa usemaji unaobagua. Majivuno anamwona Karama kama asiye na hekima kwa sababu ya weusi wa nywele zake. Kulingana na van Dijk (2006:121), miktadha ya kibaguzi huwa na usemi unaobagua; ambao unakosa upole na uteuzi wake wa maneno huwa mbaya. Katika unukuzi wa dondoo, Majivuno anamwita gharama mjinga kwa sababu ya umri wake mdogo. Ameshikilia itikadi inayohusisha hekima ya mtu na rangi ya nywele zake.

Maongezi katika riwaya kuanzia miaka ya sabini na kuendelea yametumika kutalii mada anuwai ili kupanua maudhui na kusababisha uchangamano wa msuko wa matukio. Wahusika hawazungumzii suala moja kwa kipindi kirefu bali mada hubadilika badilika kutegemea maudhui lengwa. Hali hiyo inachangia upana wa riwaya kifani na kimaudhui. Kwa mfano, katika riwaya ya *Kufa Kuzikana* (Walibora, 2003), maongezi kati ya Akida na Bwana fulani aliyemwengeza kichwa chake begani mwa Akida yanalenga kuturejesha kwa tukio la kifo cha mamake Akida (uk. 1). Ukurasa wa pili, unahusu maongezi katika mkutano wa hadhara ya kisiasa ambapo suala la ukabila linadhihirika. Kufikia ukurasa wa tano, maongezi baina ya mashabiki katika kikao cha kusikiliza mchezo wa kandanda yanaibuka. Ni muhimu kutambua kuwa, mada zinazozungumziwa zinabadilika badilika na wazungumzaji nao wanabadilika badilika. Hivyo, katika maongezi hayo, msuko na maudhui yanajengwa kwa mapana zaidi. Mtunzi anawapa usemi wahusika mahususi ili kujenga mawazo muhimu na kwa kufanya hivyo humjenga mhusika wake mkuu kwa mapana zaidi.

Maongezi katika riwaya ya *Mafuta* (1984) yanahusisha matumizi ya sitiari. Dhana za mafuta na maji zimeshamiri katika mazungumzo ya wahusika kurejelea udanganyifu na ukweli mtawalia. Sitiari hizo zinatumika ili kubainisha itikadi zinazopendelea matajiri na kudhalilisha maskini. Kulingana na Mayr na Machin (2012:164), sitiari zinaweza kuwa na mwelekeo wa kiitikadi. Hivyo, sitiari zinazokubalika zinaweza kuathiri jinsi watu wanvyofikiria, wanavyoelewa ulimwengu wao na wanavyotenda. Wasio na mafuta hawapewi fursa ya kupata rasilimali au uongozi katika jamii yao. Kitanda ni ishara ya ufanisi ambapo nafasi hiyo imepewa wateule peke yao. Mazungumzo kati ya Mtue na Msati yanabainisha hali hiyo:

*“Utawezaje kukalia bila mafuta? Ni kwa sababu huna, ama uwezo wako wa kuyapata ni haba?” akamwuliza.*

*“Si kwa sababu hiyo”, Mtue akamjibu.*

*“Ni kwa sababu gani basi?” Mtue akakaza.*

*“Na hiii... ndivyooo...! Utafanyaje?” Msati akawa anamkazania Kumwuliza (Mkangi, 1984:8).*

Maongezi katika dondoo yanabainisha ubaguzi uliopo dhidi ya wale wasiokuwa na uwezo. Hawapewi nafasi ya kukikalia kitanda ambacho ni ishara ya mafanikio. Ubaguzi ni njia mojawapo ya udhalimu kama inavyodhihirishwa na nadharia ya Uchanganuzi wa Usemi Hakiki. Matumizi ya mbinu kama vile sitiari yanachangia katika kubainisha mahusiano baina ya wanajamii. Kulingana na Paltridge (keshatajwa) Nadharia ya Uchanganuzi wa Usemi Hakiki inabainisha masuala ya kijamii, kisiasa na kitamaduni kupitia matini. Kwa mfano, katika riwaya ya *Mafuta*, kuna semi ambazo zinadhihirisha utengano wa kitabaka:

*...ni vita vya wateule; na hii ni kawaida kwani majembe hayaachi kugongana yakiwa pamoja... (Mkangi, 1984: 23).*

Usemaji ulionukuliwa katika dondoo unaendeleza itikadi za kibaguzi. Unaonyesha kuwa si vibaya wateule kuzozana wenyewe kwa wenyewe ila wasiwe na uhusiano wowote na wale wa tabaka la chini. Riwaya za Kiswahili kuanzia miaka ya sabini hadi sasa zilianza kujumuisha uchangamano wa

kimaudhui na kifani katika kukuza maongezi ya wahusika. Matumizi ya mbinu kama vile sitiari iliawezesha wahusika kuzungumzia masuala nyeti katika jamii zao kwa urahisi. Matumizi ya mbinu za kintindo anuwai yalichangia katika kufanikisha uchangamano wa riwaya ya Kiswahili.

Jambo lingine linalobainisha riwaya za miaka ya 1950 hadi 1970 ni hali ya mwandishi kutoa maelezo mafupi kabla ya kuwapa wahusika wake nafasi ya kuzungumza. Kuna matumizi ya maneno kama vile: ‘akasema’, ‘alijibu’, ‘alisaili’, ‘kisha alijibu’, ‘ndipo alipozidi kusema...’ na kadhalika. Mtunzi aliyadhibiti yaliyosemwa na wahusika na jinsi walivyoyasema. Pia, mwandishi angeweza kueleza ishara alizodhihirisha mhusika kuambatanisha na usemaji wake. Maelezo haya yanaonekana kama maelekezo ya jukwaa katika tamthilia. Kwa mfano, katika riwaya ya *Utubora Mkulima*, maongezi yafuatayo yanaibuka:

*Ahmed alimkazia macho akanena, “Wadhani mama yako angalikubali kusudi lako kama angalikuwa mzima?” (Shaaban, 1968:5).*

Mfano wa pili unapatikana katika ukurasa wa sita:

*Kwa uvumilivu mwingi Ahmed alitabasamu akanena, “Sifu jambo ulipendalo kwa sifa upendayo, lakini matokeo yake huwa mamoja siku zote (Shaaban, 1968:6).*

Katika nukuu hizo, kauli kama vile, ‘alimkazia macho’ na ‘kwa uvumilivu mwingi’ ni hali ya mwandishi kujaribu kusawiri hisia za wahusika wake. Mwandishi hakuwapa wahusika wake nafasi ya kubainisha hisia zao kutokana na usemaji wao. Kulingana na nadharia ya Uchanganuzi wa Usemi Hakiki, uhusiano wa kimamlaka unaweza kutathminika kwa kuchunguza ni nani ndiye anayadhibiti mazungumzo na anawaruhusu watu wepi kuzungumza (Paltridge, 2006:178). Katika riwaya nyingi za kipindi hicho mwandishi aliingilia kati sana mazungumzo kati ya wahusika wake. Kutokana na kuingilia kwa mtunzi katika usemaji wa wahusika, mtunzi alipata nafasi ya kuyapeleka mazungumzo kwa njia ambayo angetaka yawe. Pia, ilimsaidia mtunzi kujenga sifa za uadilifu wa mhusika alizolenga kubainisha.

Riwaya za miaka ya 1990 hadi sasa, zinahusisha aina mbalimbali za maongezi. Hivi kwamba,

mwandishi anaweza kuingilia kati mazungumzo ya wahusika wake kwa kutoa vielekezi au kuwapa wahusika nafasi ya kusema bila kutoa vielekezi. Anapowapa wahusika nafasi ya kusema bila kuingilia, msomaji anapewa nafasi ya kutambua msemaji wa usemi fulani. Kwa mfano, katika riwaya ya *Kufa Kuzikana*, kuna mazungumzo kati ya Mzee moja na mashabiki wa kandanda:

“Nini?” mzee mmoja aliwauliza.

“Tumemwona mtu”.

“Mbakaji?”

“La!”

“Mtu gani?”

“Amekufa”.

“Nani?”

“Yuko wapi?” (Walibora, 2003:4).

Katika mazungumzo kwenye dondoo, mwandishi hajataja wasemaji moja kwa moja lakini msomaji anaweza kuwatambua kutokana na jinsi wanavyosema. Kila mstari katika nukuu inahusisha usemaji wa mhusika bainifu.

### **Dhima ya Maongezi katika Riwaya za Miaka 1970 hadi Sasa**

Dhima ya maongezi inaendelea kupanuka kutokana na kukua kwa riwaya ya Kiswahili. Makala hii imebainisha kuwa, riwaya za awali ziliegemea zaidi kusawiri uadilifu wa wahusika. Hali hiyo ilifanya riwaya hizo kuwa na maongezi sahili kwa kuwa wahusika wangezungezia suala moja mara kwa mara. Hata hivyo, maongezi katika riwaya kuanzia miaka ya sabini na kuendelea yanachangia uchangamano wa msuko wa matukio na maudhui katika riwaya ya Kiswahili. Hali hii ni kinyume na riwaya za nyakati za awali ambapo maongezi yalilenga zaidi kumjenga mhusika na maudhui ya kimaadili kama alivyotaka mtunzi. Tukitumia mfano wa riwaya ya *Kufa Kuzikana* (2003), mwandishi ametumia maongezi kutekeleza dhima zifuatazo:

### **Maongezi na Ujenzi wa Mgogoro**

Kupitia usemaji wa wahusika wa riwaya, tunaweza kutambua mgogoro uliopo. Usemaji wa wahusika unasaidia kuendeleza mgogoro na kwa kufanya hivyo, husukuma mbele usimulizi katika riwaya. Mgogoro uliopo baina ya Wakorosho na Wakanju ni wa kikabila. Ukabila unasababisha uhasama baina ya makabila haya mawili jambo ambalo linasababisha mauaji ya halaiki. Ili kujenga uhasama wa kikabila, mtunzi anaibua maongezi baina ya wahusika ili kubainisha misimamo yao kuhusu masuala yanayohusu ukabila. Kwa mfano, katika mkutano wa hadhara, mbunge Johnstone Mabende ananukuliwa akisema kuwa, hawakutaka ‘madoadoa’ katika eneo hilo. Neno ‘madoadoa’ linawarejelea Wakanju ambao hawakuwa wakaazi asilia wa eneo hilo. Uzungumzaji wa Mabende ni wa kibaguzi unaodhihirisha jinsi uhusiano kati ya Wakanju na Wakorosho ulivyokuwa. Kauli hiyo ya Mabende inasababisha maongezi kati yake na mwalimu Alex ambaye anawaona Wakanju kama ndugu zao. Hapa mwandishi anadhihirisha misimamo tofauti kuhusu suala la ukabila katika eneo hilo. Wanaomuunga mkono mbunge Mabende wanamwona mwalimu Alex kama msaliti. Pengine kauli ya mwalimu Alex ndiyo inayosababisha kifo chake jambo ambalo linatumia kuhlalisha vita baina ya Wakanju na Wakorosho.

Mwandishi badala ya kutumia mbinu ya masimulizi ya moja kwa moja anaibusha maongezi kati ya wahusika wake ili kudhihirisha uzito wa suala linaloibua mgogoro. Kupitia maongezi ya wahusika, misimamo yao kuhusu mambo mahususi yanabainishwa. Katika kikao cha kusikiliza kandanda redioni, mashabiki wa kandanda wanaanza kupingana kwa kuwanasibisha wachezaji na makabila yao:

“Wale ni Wakorosho bwana”.

Timu ya taifa si timu bila Wakorosho yakhe”.

“Hapana”, alibisha Mkanju. “Chewa si Mkorosho, ni Mkanju. Tangu lini Wakorosho wakajua kufunga goli?”

“La! Ni Mchungwachungwa, alisoma na dadangu chuoni”, alisema mwingine.

“Dadako gani aliyesoma hata shule ya chekechea? Usiturubuni bure bwana; hamna mtu wa kwenu Uchungwani anayeweza walau

*kuandika jina lake mwenyewe*". (Walibora, 2003:4).

Mazungumzo yaliyonukuliwa katika dondoo yanaonyesha kauli za kibaguzi. Ubaguzi unaodhihirika katika muhtadha huo ni wa kikabila. Hivyo, inakuwa rahisi kwa Wakanju na Wakoroshu kupigana kutokana na chukulizi walizokuwa nazo kuhusu kabila nyenziye. Kulingana na van Leeuwen (2008:106) wanajamii wanaweza kutekeleza uhalalishaji wa matendo fulani kwa kurejelea utamaduni, mila, sheria au watu wenye mamlaka katika jamii. Uhalalishaji wa aina hiyo unadhihirika katika mazungumzo kati ya mashabiki wa kandanda kutoka jamii za Wakoroshu, Wakanju na Wachungwachungwa. Kwa mfano, wanatumia michezo na elimu kudhalilishana kikabila. Uhalalishaji wa aina hiyo unaibua chukulizi zisizo na mantiki kuhusu watu wa jamii nyingine.

### **Maongezi na Tofauti ya Kimazingira**

Katika kubainisha tofauti ya wahusika kwa mujibu wa welewa wao kuhusu mazingira mapya, mwandishi anaibua maongezi kati yao. Maongezi haya yanaweza kuonyesha kutojua au kujua kwa wahusika. Kwa mfano, katika riwaya ya *Kufa Kuzikana*, mwandishi anaonyesha tofauti baina ya wahusika wa mjini na mashambani kupitia mazungumzo kati yao. Akida anapomtembelea Tim mjini anabainisha kutojua kwake kupitia maongezi yao mle mkahawani. Anadhani kuwa '*chips*' ni samaki na '*sausage*' ni chuchu za ng'ombe. Maongezi kati ya wahusika yanatekeleza dhima ya kumfanya msomaji kumwelewa zaidi mhusika kwa kumhusisha na hali yake.

Wakaazi wa mashambani wanaonekana kutoelewa mambo mengi ya mjini. Kuna kichekesho kuhusu bwana moja aliyeenda mjini na kukasirika kwa kutojibiwa na wafanyakazi katika duka la Baniani. Ili kudhihirisha hali ilivyokuwa wakati wa tukio hilo, mwandishi anawapa wahusika wake nafasi ya kusema:

*"Iko nini baya?" Baniani alimsaili.*

*"Hawa wafanyakazi wako mbona nawauliza bei ya nguo, wananikodolea tu macho?"*

*"Veve mtu gani hii?" alimaka baniani. Pana jua dummy? Hii pana mutu naveza kujibu veve;*

*sanamu tu sisi navalisha nguo"* (Walibora, 2003:9).

Maongezi kama hayo kwenye dondoo yanazidisha uhai wa kisa. Kichekesho chenyewe kinadhihirika zaidi hasa kinaposemwa moja kwa moja kama kilivyosemwa na wazungumzaji asilia. Pia, maongezi hayo yanaonyesha jinsi matumizi ya lugha yanavyoweza kubainisha sifa za asili na tabaka la mhusika. Bwana asiyejua kuhusu sanamu anajibagua kupitia kwa usemi wake mwenyewe. Anadhihirisha kuwa, alikuwa mgeni kule mjini hivyo; hakujua kuhusu sanamu zinazovalishwa nguo kwenye milango ya maduka kubwa.

### **Maongezi na Ujenzi wa Msuko wa Matukio**

Mwandishi anaweza kutumia maongezi ya wahusika kupeleka mbele visa na vitushi katika riwaya yake. Uchangamano wa msuko wa riwaya unaweza ukazuliwa na kukuzwa kupitia maongezi ya wahusika. Kupitia maongezi, mwandishi anaweza kuturejesha nyuma kwa tukio la awali au kujenga hali ya taharuki katika msuko wa riwaya. Maongezi yanakuwa kama daraja la kujenga visa na vitushi mahususi katika riwaya husika. Hii ina maana kuwa, kauli za mhusika zinaweza kutumiwa kama kichocheo cha kukumbuka matukio yaliyotokea kitambo au kuacha katika hali ya kutufanya kutamani kujua hatima yake. Pia, uzungumzaji kati ya wahusika unaweza kuwa kisababishi cha kutendeka kwa tukio ambalo linasukuma mbele usimulizi wa riwaya. Hii ina maana kuwa usemaji wa wahusika huweza kumfanya mhusika mwenzake kutenda tendo fulani, ambalo linasababisha matendo mengine. Wingi wa matendo yanayosababishwa na usemaji hukuza upana na uchangamano wa riwaya ya Kiswahili. Kutokana na dhima hii ya maongezi, baadhi ya riwaya za kipindi cha karne ya 21 zina maongezi mengi kwa malengo ya kutekeleza majukumu anuwai.

Kwa mfano, katika riwaya ya *Kufa Kuzikana*, msimulizi anamwuliza abiria anayeketi karibu naye kuhusu vilima alivyoviona. Anapojibiwa kuwa ni Tungule, anaturejesha nyuma kwa tendo la kufa kwa mamake. Hapa ndipo tunapojuzwa kuwa mamake Akida alikufa kutokana na ajali ya barabara katika milima hiyo ya Tungule. Hivyo, maongezi haya yametumika kama kichochezi cha



kumbukumbu ya msimulizi kuhusu kifo cha mamake.

Mazungumzo baina ya Sululu na Zablon (uk.5) yametumiwa kuonyesha uhasama wa kikabila katika eneo la Baraki. Maongezi haya ndiyo yanayotujulisha kuwa ilani zilikuwa zimesambazwa kuwa Wakanju wahame eneo la Korosho. Hata hivyo, badala ya kuendeleza mazungumzo haya mwandishi anajenga taharuki kuhusu matokeo ya kusambazwa kwa ilani hizo. Tunasimuliwa kuhusu matayarisho ya msimulizi kwa sherehe za kuwatuza wanafunzi bora ambayo ingeongozwa na Waziri wa Elimu. Tunaweza kudai kuwa maongezi baina ya Zablon na Sululu yametumiwa kuongeza hamu ya msomaji kuendelea kusoma riwaya ili kujua yatakayofanyika baadaye. Mfano wa maongezi yanayotekeleza dhima ya kusababisha kitendo kingine, ni yale yanayotokea katika klabu ya pombe. Mzee Tito Tembo anajisifia kwa wanywaji wenzake jinsi alivyowaua Wakanju wengi. Anasema:

*“Mwenyewe mimi usinione hivi nimeua Wakanju wengi sana”, alijipigapiga kifua. “Usione wembamba wa reli, garimoshi hupita” (Walibora, 2003:5).*

Usemaji wa Tito Tembo unaibua hasira za Akida. Hii inamfanya Akida kumpiga Tito bao na kudhani kuwa amemua. Tukio hilo linamfanya Akida kutorokea eneo la Sangura anakoenda kufanya kazi katika shamba la Mzee Muyaka. Hivyo basi, tunaweza kudai kuwa usemaji wa Tito Tembo unakuza upana wa riwaya kwa kusababisha vitushi vinginevyo.

Aidha, maongezi yanajenga msuko wa riwaya kupitia kwa mtindo wa taharuki. Mbinu hii huzua hamu ya msomaji kutamani kujua kitakachofuatia. Pam anapomwambia Akida kuwa, ‘Anamwonea fahari’ (uk. 48). Inamfanya Akida kudhani kuwa Pam alikuwa akimpenda. Mtazamo wa Pam kuhusu Akida unacheleweshwa hata baada ya Pam kutoa kauli hiyo. Je, Pam anampenda Akida kweli? Kwa kufanya hivi, msomaji naye anakanganyika ikiwa kweli Pama anampenda Akida. Hata Tim mchumbake Pam anakanganywa. Ni mwisho mwisho wa riwaya ndipo tunapojuzwa kuwa kuwa Pam alikuwa akitaka urafiki tu na Akida.

### ***Maongezi na Ujengaji Hali Halisi***

Kazi ya riwaya ni bunilizi. Hata hivyo, riwaya wakati mwingi hulenga kusawiri matukio maalum katika jamii. Ili kuandika mambo ya kuaminika kwa msomaji, wakati mwingine mwandishi hutumia maongezi kwa namna ambayo maongezi hayo yanafanana na mazungumzo ya kawaida miongoni mwa wanajamii. Maongezi yanafanya wahusika na miktadha mbalimbali kuwa ya kuaminika. Kuna mazungumzo yanayotokea kati ya Tim na Akida hotelini katika ukurasa wa 13 hadi 15. Mazungumzo yanabadilika badika kutokana na kuathiriwa na yanayoendelea katika mazingira yao. Kwa mfano, kufika kwa mhudumu wa hoteli kunahamisha mazungumzo yao kutoka yale yanayowahusu wazazi wao hadi yanayohusu vinywaji. Pia, Akida anapomwona David aliyekuwa akim dai anahamisha mazungumzo na kuanza kuzungumza kuhusu deni lake. Kukatizwa kwa mazungumzo na kisha kurejelewa baadaye yanafanana na mazungumzo yalivyo kwa kawaida katika jamii. Kwa kujenga mazungumzo ya aina hiyo, mwandishi anasawiri uhalisia wa mazungumzo ya kawaida katika jamii.

### **HITIMISHO**

Makala hii imetofautisha maongezi katika riwaya za 1950 hadi 1970 na zile za 1990 hadi sasa. Waandishi wa makala hii wametumia mifano kutoka riwaya za; *Kusadikika* (1951), *Mafuta* (1984) na *Kufa Kuzikana* (2003). Kutokana na maelezo tuliyotoa ni bayana kuwa maongezi yana nafasi kubwa katika kujenga msuko na upana wa riwaya. Makala hii imedhihirisha kuwa, wahusika katika riwaya za miaka ya 1950 hadi 1970 aghalabu walizungumzia suala moja tu. Waandishi wa riwaya hizo walilenga kumkuza mhusika mwadilifu aliyekuwa kielelezo cha kuigwa na wanajamii. Hivyo, usemaji wa mhusika mkuu na wahusika wengine ulilenga kutimiza dhamira hiyo ya mwandishi. Kutokana na hali hiyo, maongezi katika riwaya hizo yalikuwa sahili na hayakujumuisha mbinu anuwai za kintindo. Riwaya za kuanzia miaka ya sabini zimedhihirisha maongezi changamano. Uchangamano wa maongezi hayo unatokana na wahusika kuzungumzia masuala mengi ya kijamii, kisiasa na kiuchumi. Aidha, watunzi wa riwaya hizo wamejumuisha mbinu za kitamathali katika maongezi ya wahusika ili kusawiri mahusiano muhususi katika jamii.

**MAREJELEO**

- Bakhtin, M. (1989). *The Dialogic Imagination*. Austin: University of Texas Press.
- Bolinger, D. (2014). *Language - The Loaded Weapon: The Use and Abuse of Language Today*. London: Routledge.
- Celce-Murcia, M. na Olshtain, E. (2000). *Discourse and Context in Language Teaching: A Guide for Language Teachers*. Cambridge: Cambridge University Press.
- Fairclough, N. (1992). *Discourse and Social Change*. Cambridge, UK: Polity Press.
- Haines B. (1991). *Dialogue and Narrative Design in the Works of Adalbert Stifter*. London: Modern Humanities Research Association.
- Hawthorn, J. (1992). Studying the novel: An Introduction. (2<sup>nd</sup> ed). London: Hodder/ Arnold.
- Kezilahabi, E. (1990). *Nagona*. Dar es Salaam: Dar es Salaam University Press.
- Mayr, A. na Machin, D. (2012). *How to Do Critical Discourse Analysis: A Multimodal Introduction*. London: sage.
- Mbotela, J.J. (1934). *Uhuru wa Watumwa*. London: Sheldon Press.
- Mkangi, K. (1984). *Mafuta*. Nairobi: Heinemann Educational Books.
- Mohamed, S.A. (2001). *Babu Alipofufuka*. Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation.
- Mohamed, S.A. (2003). "Fragmentation, Orality and Magic Realism in Kezilahabi's Novel Nagona." *Nordic Journal of African Studies*, 12(1). 78 – 91.
- Mohamed, S.A. (2006). *Dunia Yao*. Nairobi: Oxford University Press, East Africa Ltd.
- Mohamed, S.A. (2007). "Vionjo vya Riwaya Mpya ya Kiswahili." *Kioo cha Lugha*, 5(1), 11–17. Retrieved from <http://dx.doi.org/10.4314/kcl.v5i1.61424>.
- Mwamzandi, I. (2013). "Riwaya Teule za Karne ya Ishirini na Moja na Udurusu wa Nadharia za Fasihi." *Swahili Forum*, Vol. 20, 48 – 66.
- Paltridge, B. (2006). *Discourse Analysis: An Introduction*. London: Continuum.
- Robert, S. (1951). *Kusadikika*. Nairobi: East African Literature Bureau.
- Robert, S. (1952). *Adili na Nduguze*. London & Basingstoke: Macmillan Publishers.
- Robert, S. (1967) *Kufikirika*. Nairobi: Oxford University Press.
- Robert, S. (1968). *Utubora Mkulima*. Nairobi: Evans Brothers Ltd.
- Robert, S. (1968). *Siku ya Watenzi Wote*. Nairobi: Nelson.
- Van Dijk, T. (1998). *Ideology: a multidisciplinary approach*. London: Sage.
- Van Dijk, T. (2006). "Ideology and Discourse Analysis." *Journal of Political Ideologies* 37(2), 115 -140. doi:10.1080/13569310600687908.
- Van Leeuwen, T. (2008). *Discourse and Practice: New Tools for Critical Discourse Analysis*. Oxford: Oxford University Press.
- Walibora, K. (2003). *Kufa Kuzikana*. Nairobi: Longhorn Publishers.
- Wamitila, K.W. (2006). *Uhakiki wa Fasihi: Misingi na Vipengele Vyake*. Nairobi: Phoenix Publishers.
- Wodak, R. (2001). What CDA is about – a summary of its history, important concepts and its developments. Katika R. Wodak and M. Meyer (Wah.) *Methods of Critical Discourse Analysis* (uk. 1 – 13). London: Sage.
- Wodak, R. (2001). The discourse – historical approach. Katika R. Wodak and M. Meyer (Wah.), *Methods of Critical Discourse Analysis* (uk. 63 – 94). London: Sage.